Kwa mfano: kutoa huduma endelevu ya usambazaji wa maji kwa kuzingatia dhana ya uendeshaji na matengenezo.

Muongozo unafafanua zaidi dhumuni la Chombo kuridhia kuanzishwa kwa mpango wa biashara wa miaka mitatu . Mpango huu utanza mwaka 2021/22 hadi mwaka wa fedha wa 2023/24 kwa kufuata muongozo uliotolewa na mdhhibiti wa vyombo vya watoa huduma ngazi ya jamii, RUWASA.

2.0 Maelezo Kuhusu Chombo

2.1 Muundo wa Jumuiya ya Maji

Kamati ya Jumuiya ya Watumia Maji itaundwa na idadi ya watu 9 kama walivyoainishwa hapo chini. Miongoni mwa wajumbe wapo wale wa wakuchaguliwa na wengine wanaaingia kulingana na nyadhifa zao za uongozi katika Kata.Kamati ya Chombo husika itahudumu kwa muda wa miaka XXX. Muundo

wa Kamati ya Maji iliyopo madarakani, kuanzia lini na majina yao kwa nafasi zifuatazo: - (Ukomo wa uongozi, vyeo na nafasi za uongozi ndani ya Chombo)

Nafasi zitakazo unda kamati ya Jumuiya ya Watumia Maji ni kama ifuatavyo:

- Mwenyekiti
- Katibu
- Mjumbe – (Mtendaji wa Kata)
- Mwakilishi wa wanawake
- Mwakilishi wa watumiaji maji
- Mheshimiwa Diwani Kata
- Mwakilishi wa zahanati
- Mwakilishi kutoka shule
- Mwakilishi wa mtendaji wa kijiji



2.2 Hali ya Watumishi

Chombo kitaeleza idadi ya watumishi waliopo na nafasi zao za ajira. Kwa mfano; utumishi wa mkataba, kudumu au kibarua. Iwapo ni mtumishi wa mkataba basi ifafanuliwe vipengele vyote muhimu vya majukumu na muda wa mkataba. Taarifa muhimu za watumishi wote zitapaswa kuandaliwa na kutunzwa vizuri ikiwa ni pamoja na orodha, fani, na viwango vya elimu yao kwa ufafanuzi zaidi.



2.3 Idadi ya Watu katika Eneo La Huduma

Chombo kitatakiwa kuwa na taarifa za msingi za eneo kinako toa huduma kwa mfano, idadi ya vijiji na jumla ya idadi ya watu wanaohudumiwa.



2.4 Mahitaji ya Maji na Uzalishaji



Ni muhimu muda wote Chombo kiwe na taarifa zinazo husiana na mahitaji ya maji kwa wakazi wa kijiji/vijiji kinamotoa huduma. Taarifa hizo ni pamoja na asilimia (%) ya watu ambao tayari wanapata maji kwa wakati huo, wanaohitaji na wale waliokwenye mpango wa kuunganishiwa huduma ya maji. Pia, Chombo kinao wajibu wa kwenda mbele zaidi na kuhakikisha kinakuwa na taarifa na kumbu kumbu ya maji yanayozalishwa au kupotea katika harakati za kuzalisha na kusambaza. Kumbu kumbu hizi zinaweza kutafsiriwa katiaka asilimia kwa vipindi tofauti kama vile wiki, mwezi, robo ya mwaka, nusu ya mwaka na kwa mwaka mzima.

2.5 Vyanzo vya Maji

Chombo kinatakiwa kuvibaini vyanzo vyote vya maji vilivyomo kwenye eneo husika. Vyanzo vitathiminiwe kwa kulinganisha uwezo wake wa kuzalisha maji na mahitaji ya watumiaji. Vyanzo vitajwe kwa idadi, sifa na pale ambapo vyanzo havitoshelezi mahitaji basi Chombo kitoe mapendekezo mbadala ya suluhisho. Vyanzo mbadala yaweza kuwa vimeendelezwa au bado havijaendelezwa.

2.6 Mitambo ya Kusukumia Maji

Maji hufikishwa kwa watumiaji kupitia mifumbo mbali mbali kulingana na aina ya chanzo na sababu nyingine nyinginezo za kiufundi. Chombo kinashauriwa kuitambua mitambo yake kwa kuangalia vigenzo mbali mbali kama vile aina ya mitambo/pampu zilizopo, mahali zilipo, idadi na uwezo wake.

2.7 Vituo vya Kusukumia Maji

Iwapo Chombo kinavyo vituo vya kusukumia maji, ni vema kuhakikisha pia uwepo wa taarifa muhimu kama vile idadi ya vituo, utoshelevu au upungufu wa maji kulinganisha na hali na sifa za vituo vya kusukumia maji. Ili kuwezesha mipango, maamuzi na utendaji ni vema pakawepo na taarifa zenye

kuonyesha viwango halisi vya maji yanayosukumwa.

2.8 Matenki ya Kuhifadhia Maji

Uhifadhi wa maji sio tu kuwa no moja ya vipaumbele vya kila Chombo bali mkakati wa makusudi katika kuhakikisha uhakika wa upatikanaji wa huduma. Hivyo hali na idadi ya matenki ni lazima viwekwe bayana sambamba na uwezo wa ujazo wa matenki hayo

2.9 Mtandao wa Mabomba ya Maji

Chombo kinapaswa kuzingatia masuala ya msingi katika kuratibu mtandao wake wa mabomba kama vile urefu, aina ya mabomba yaliyotandazwa na hali yake.

2.10 Wateja wa Maji

Wateja wamegawanyika katika makundi mbali kulingana na mahitaji ya maji na shughuli zao za kijamii na kiuchumi. Hivyo, Vyombo vinahimizwa kuwa kuweka taarifa sahihi za wateja zikiwa zimeainishwa kwa kuzingatia mtawanyiko wake. Mambo ya kuzingatia ni pamoja na jumla kuu ya wateja, idadi ya wateja kwa kwa kila kundi na tabia za kila kundi katika matumizi ya maji. Taarifa hizi zinapaswa kuchukukulia kila baada ya vipindi maalum.

Kwa mfano; Jumuiya ya watumia maji hadi kufikia mwezi XXX mwaka XXX, imekuwa na jumla ya wateja kama ifuatavyo: -:-

- Majumbani	
- Biashara	
- Taasisi	
- Magati	
JUMLA KUU	

2.11 Viwango vya Ubora wa Huduma ya Maji Itolewayo



Chombo chochote cha Huduma ya Watumiaji Maji nchini kinaongozwa na sheria na miongozo inayoratibiwa na RUWASA. Hivyo basi. Hali ya huduma ya maji itolewayo kwa wananchi haina budi kuwa ni ya maji safi na salama kwa kiwango cha T.T.S (Tanzania Temporal Water Quality Standard).

2.12 Makusanyo ya Mapato na Matumizi



Ili kutathmini ufanisi, utengamavu na uendelevu wa Chombo ni vema kukazingatiwa dhana ya uwazi na ukweli. Vitabu vya mahesabu vitalazimika kuweka bayana makusanyo yote ambayo ni mapato ya Chombo. Yapo masuala ya kuzingatiwa katika udhibiti wa mapato na matumizi. Jumuiya inalazimika kuwasilisha wastani wa mapato na matumizi kwa kila mwaka. Taarifa ya mapato na matumizi lazima ionyeshe muda maalum inamowasilishwa, kwa mfano mapato na matumizi kwa mujibu kipindi kinachoanzia mwezi XXX hadi mwaka XXX.

2.13 Maeneo Ambayo Hayajafikiwa Na Huduma



Jumuiya ya Watoa Huduma ya Maji inayo mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Katika kutekeleza mipango mikakati ya Chombo, mipango ya muda wa kati na mrefu huzingatia pia maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma. Makisio, bajeti na rasilimari huandaliwa ili kutengeneza mazingira ya kupanuliwa kwa miradi na huduma za maji. Vijiji/mitaa ambayo haijafikiwa kabisa na huduma itatambuliwa kwa majina, idadi ya watu, mahitaji ya maji na miundo mbinu yake ili kuweza kusaidia kufanya maamuzi ya utekelezaji wa miradi.

2.14 Miradi ya Maji Iliyopo

Jumuiya ya Watoa Huduma ya Maji inatazamiwa kuwa na ripoti inayo akisi miradi yote ya maji iliyopo kwa wakati husika. Miradi ya maji itatambuliwa kwa hali halisi iliyonayo kwa kipindi

inaporipotiwa. Kwa mfano, miradi inayofanya kazi vizuri, miradi inayo sua sua, miradi iliyo kwenye ukarabati, ujenzi na hatua zake na hata ile iliyotelekezwa.

3.0 Maono na Dhima


3.1 Maono

Inashauriwa kuwa kila Chombo kinapaswa kuwa na maono ili kukiwezesha kubuni na kutekeleza mipango yake pasipo kukiuka malengo ya msingi. Kwa kuwa na maona yanayotekelezeka, Chombo kinaweza kukadiria mahitaji ya muda, fedha, watu na zana zinazohitajika kutimiza mahitaji yake. Kwa mafano, "Chombo kina matamania ya kuwa miongoni mwa Watoa Huduma ya Maji ngazi ya jamii chenye uwezo wa kutoa huduma bora ya maji safi na usafi wa mazingira Tanzania Bara"



3.2 Dhima

Usahihi wa muelekeo na nia ya uanzishwaji wa Chombo cha Watoa Huduma ya Maji ngazi ya jamii hutambulika kupitia dhima waliyo nayo. Utendaji kazi wa watumishi na uamuzi wa mipango ya Chombo huwa rahisi kufuatia usahihi wa dhima. Kwa mfano, "Jukumu la msingi la chombo ni kutoa huduma ya maji safi, salama na ya kutosha, gharama nafuu kwa wateja wetu kila siku kwa masaa 24.



4.0 Malengo Mahususi ya Chombo Kwa Mwaka

Malengo mahususi hukisaidia Chombo kupanga kwa ustadi na uhakika kazi za miradi kwa kuzingatia mikakati kilichojiwekea. Malengo haya huenda mbali hadi kuweza kubainisha kiwango halisi cha mahitaji ya rasilimali kama vile watu, muda, fedha na zana za kazi. Ndani ya mwaka mpango wa mwaka mmoja huweza kutawanywa katika vipindi tofauti ikiwemo malengo ya wakati ujao.



Malengo ya Chombo yako yaaina mbili:

- (a) Malengo ya kuboresha huduma ya maji
- (b) Malengo ya kuboresha viwango vya huduma ya maji.

4.1 Malengo ya Kuboresha Huduma ya Maji

Jedwali Na: 1 Ni mfano wa uchambuzi wa matarajio ya kuboresha huduma ya maji kwa miaka mitatu ijayo ambavyo pia inalenga katika kukipandisha Chombo daraja

Jedwali Na. 1: Malengo ya Kuboresha Huduma ya Maji

Na	Maelezo	Mwaka wa Sasa (M)	M+1	M+2	M+3
1.	Watu wanaohudumiwa na maji (%)	40	50	70	80
2.	Uwiano wa maji yanayozalishwa na mahitaji (%)	45	55	75	60-74.9
3.	Ufanisi wa kukusanya Mapato (%)	40	50	70	80
4.	Uwiano wa matumizi na mapato (Working Ratio (WR))	1.2	1.1	=1	0.9
5.	Ufungaji wa dira za maji (%)	50	60	70	75
6.	Maji yanayopotea (NRW (%))	40	38	35	30
7.	Saa za utoa uduma (Hrs)	5	6	7	9
8.	Kukidhi iwango vya bora wa aji (%)	30	60	70	80
9.	Kukidhi vigezo vya sheria (Compliance to Statutory Requirements (%))	30	50	65	80
10.	Pop saved with HHC (%)	10	20	30	35

4.2 Malengo ya Kuboresha Viwango vya Ubora wa Huduma ya Maji

Jedwali Na: 2 Ni mfano wa uchambuzi wa matarajio ya utekelezaji wa viwango vya ubora wa huduma kama ilivyoanishwa kwenye mkataba wa Chombo na wateja.

Jedwali Na. 2: Malengo ya Kuboresha Viwango vya Ubora wa Huduma ya Maji

Na	Ubora wa Huduma	Viwango vya Sasa (M) vya Ubora wa Huduma	Matarajio ya Viwango vya Huduma kwa Mwaka 2021/22 hadi 2023/24		
		(M)Mkataba wa Huduma wa Wateja	M+1	M+2	M+3
1.	Upatikanaji wa huduma	Saa 12	Saa 15	Saa 18	Saa 22
2.	Ubora wa maji	Kulingana na viwango vya TBS	Kulingana na viwango vya TBS	Kulingana na viwango vya TBS	Kulingana na viwango vya TBS
3.	Muda wa kuchunguza malamiko ya ankara za maji	Siku 5	Siku 5	Siku 3	Siku 2
4.	Muda wa kuchunguza malamiko yasiyohusu ankara za maji	Siku 15	Siku 15	Siku 12	Siku 10
5.	Kuunganisha wateja wapya wa majumbani baada ya kulipia gharama zote	Siku 7	Siku 7	Siku 5	Siku 4
..	..	..	..	..	..

6.	Usomaji wa dira za maji	Mara moja kwa mwezi	Mara moja kwa mwezi	Mara moja kwa mwezi	Mara moja kwa mwezi
7.	Kurekebisha/ kubadilisha dira ya maji yenye matatizo	Siku 30	Siku 25	Siku 20	Siku 15
8.	Kusoma mita, kuandaa na kusambaza nkara za maji	Tarehe 15 hadi tarehe 21 ya kila mwezi	Tarehe 15 hadi tarehe 21 ya kila mwezi	Tarehe 15 hadi tarehe 21 ya kila mwezi	Tarehe 15 hadi tarehe 21 ya kila mwezi
9.	Kurudishia huduma ya maji kwa wateja waliokatiwa baada ya kulipa	Saa 24	Saa 24	Saa 24	Saa 24
10.	Kurudishia huduma ya maji kwa wateja waliokatiwa kimakosa baada ya kupta taarifa	Saa 24	Saa 24	Saa 24	Saa 24


5.0 Uchambuzi wa Kibiashara wa Chombo

5.1 Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto

Uchambuzi wa uwezo, udhaifu, fursa na changamoto za Chombo hufanyika ili kutambua maeneo ambayo Chombo kina uwezo na fursa za kufanya vizuri na maeneo ambayo Chombo kiko dhaifu na kina changamoto ili kuweza kutambua maeneo yanayohitaji maboresho. Uchambuzi huu utafanyika kwa mfano uliopo kwenye jedwali Na: 3 hapo chini.

Jedwali Na. 3: Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto (SWOC Analysis)

Uwezo	Udhaifu
Kitu ambacho CBWSOs inafanya vizuri. Rasilimali ya CBWSos Kwa mfano: ● Inasambza maji kwa saa 24 kwa siku ● Wateja wote wamefungiwa dira za maji ● Ina mfumo wa kompyuta wa kutayarishs bili za maji	Kitu ambacho CBWSO ingeweza kufanya vizuri Kitu ambacho wateja wanalalamika dhidi ya CBWSO Kwa mfano: ● Kuchelewa kurudisha huduma ya maji kwa watu waliolipia deni ● Wateja wanakatiwa maji bila kupewa tarifa ● Asilimia kubwa ya maji yanayopotea ● Wizi wa maji ● Upungufu wa vyombo vya usafiri ● Uchakavu wa miundo mbinu ya maji ● Upungufu wa vitendea kazi ● Jumuiya haina ofisi ya kudumu ● Upungufu wa samani za ofisi
Fursa	Changamoto
Fursa zilizopo <i>Mfano:</i> ● Uwepo wa maji ya kutosha..... (taja chanzo husika). ● Ongezeko la watu katika eneo husika kama Kijiji kinapanuka kuelekea mji. ● Ukuaji wa kasi wa mji mdogo wa Ndala. ● Uwepo wa ushirikiano wa kutosha wa RUWASA na wadau wengine wa maendeleo (wataje kama wapo).	Vikwazo vilivyo nje ya CBWSO vinavyokwaza maendeleo ya CBWSO Masuala mapya yanayotokea katika sekta ya maji km mabadiliko ya sheria <i>Mfano:</i> ● Mahitaji ya kulipa gawiwo kwa serikali ● Mabadiliko ya sheria ● Mahitaji ya kukidhi vigezo vya ubora wa maji



- Uwepo wa vyanzo vya maji vya kutosha.... (kama vipo)

5.2 Mchanganuo wa Ongezeko la Watu

Chombo kitakokotoa matarajio ya ongezeko la watu katika eneo lake la huduma. Inashauriwa kwamba sensa ya taifa itumike katika kupanga matarajio ya ongezeko la watu kwa kuzingatia idadi ya watu waliohesabiwa kipindi kilichopita kutoka katika kila kijiji/mtaa. Rejea jedwali Na: 4

Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Ongezeko la wa Watu

Na	Mtaa/ Kijiji	Idadi ya Watu kwa Sasa	Asilimia ya Ongezeko la Watu (%) kwa mujibu wa sensa)	Matarajio ya Ongezeko ya Watu kwa Miaka Mitatu		
				M+1	M+2	M+3
1.						
2.						
3.						
4.						
5.						

5.3 Uchambuzi wa Matarajio ya Watu Watakaohudumiwa

Uchambuzi wa watu watakaohudumiwa katika kila mtaa/kijiji (watu wa kila mtaa na kijiji wamekokotolewa kwenye kifungu 5.2) utainishwa kwenye jedwali Na. 5. Wastani wa asilimia ya watu watakaohudumiwa katika kipindi cha miaka mitatu ioane na kiwango kilicho kwenye malengo ya kuboresha huduma (kifungu 4.1)

Jedwali Na. 5: Uchambuzi wa Matarajio ya Watu Watakaohudumiwa

Na	Kijiji/ Mtaa	Idadi ya Watu (Na) kwa Sasa	Kwa Sasa (M)			Matarajio ya Watu Watakaohudumiwa (Na) na Asilimia (%)		
			Idadi ya Watu Wana ohudu miwa (Na)	Idadi ya Watu Wasio na Hudu ma (No)	Asilimi a ya Watu Wanao pata Maji (%)	M+1	M+2	M+3
Jumla								



5.4 Uchambuzi wa Matarajio ya Mahitaji ya Maji

Mahitaji ya maji kwa mujibu wa matarajio ya watu watakaohudumiwa (5.3) yanatoa mwanga kuhusu upungufu/ziada ya maji yatakayokuwepo katika kipindi cha mpango wa kibiashara. Uchambuzi wa mahitaji ya maji kwa wateja mbali mbali utafanyika kwa kuzingatia “Maji Design Manual 2020” na utawasilishwa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali Na: 6



Jedwali Na. 6: Uchambuzi wa Matarajio ya Mahitaji ya Maji

Mwaka	Majumbani	Taasisi	Biashara	Viwanda	Vyaklula	Matumizi Mengine (Eleza)	Jumla ya Mahitaji (1+2+3+4+5+6)	Maji Yanayozalishwa 2020/21	Upungufu/Ziada ya Maji Yanayozalishwa (7-8)
	1	2	3	4	5	6	7	8	9
M									
M+1									
M+2									
M+3									

5.5 Mahusiano na Wateja

Chombo kinapashwa kuwa na mahusiano mazuri na wateja wake kwa kuhakikisha mkataba wa huduma kwa wataje unazingatiwa ikiwa ni pamoja na kutoa huduma kulingana na viwango vya ubora. Ni vema kuwa na mawasiliano mazuri na wateja ili kuepusha migogoro na kuweka vipaumbele vya kupeleka maji kwa maeneo ambayo yenye upungufu na yale yasiyo na huduma kabisa. Elezea mbinu zitakazotumika kuboresha mahusiano na wateja. (Pangewekwa mfano wa mbinu za kuboresha mahusiano badala ya kuwataka waeleze)

5.6 Mahusiano na Jamii

Chombo kinapashwa kuwa na mahusiano mazuri na jumuiia katika eneo lake la utoaji huduma. Kwa mfano watu binafsi, wawekezaji, taasisi za dini, taasisi za elimu, kambi za jeshi na

magereza. Kushindwa kukidhi matarajio ya wateja yaweza kuwa chanzo mahusiano mabaya baina ya chombo na jamii. Mawasiliano ya mara kwa mara na wadau husaidia kufahamika kwa sera, mipango na huduma za chombo kwa ujumla wake hivyo kupunguza uwezekano wa kuvunjika kwa mahusiano. Taarifa za kusambazwa mara kwa mara kwa umma ni pamoja na wajibu wa Chombo kwa wateja, bei, utaratibu wa utoaji huduma na vema Chombo kikawa na miongozo inayo ratibu upashaji habari ili kuhahakisha kuwa hapapatikani fursa ya kuhujumu juhudi za chombo. Mbinu mbali mbali zinazoweza kutumika kimarisha mahusiano ni pamoja na hizi zifuatazo:

Mikutano na vikundi mbalimbali (madiwani na wabunge, walimu wa shule, viongozi wa dini, viongozi wa mitaa nk).

- Kuwasilisha mada kwenye vyombo vya habari kamaradio, television
- Kutoa machapisho kwenye magazeti,
- kutumia mitandao ya kijamii kama vile Facebook, whatsapp, twitter na histogram
- Kutengeneza vipeperushi nk.

6.0 Uchambuzi wa Hali ya Miundombinu

Ili kuweza kutoa huduma endelevu kunategemea hali na uwezo wa rasilimali na miundo mbinu inayotumiwa. Lipo jedwali katika mada hii lenye kufafanua njia ya kuitambua na kuchambua hali ya miundo mbinu. Miundo mbinu ya kutolea huduma inatazamwa katika maeneo tofauti tofauti kama vile matengenezo, ukarabati na ununuzi wa miundo mbinu mipya. Baada ya kubaini hali halisi ya miundo mbinu na kujua mahitaji yafuatayo yanaweza kufanyika:

(a) Kufanya matengenezo ya kawaida

Iwapo miundo mbinu iko katika hali nzuri itahitaji matengezo ya kawaida ya mara kwa mara ili iendelee



kutoa huduma ipasavyo. Kwa miundo mbinu ya aina hii gharama zinazotakiwa ni matengenezo ya kawaida na makisio yatafanyika kwa kila kipindi cha miaka mitatu.

(b) **Kukarabati au kubadilisha vipuri vya miundo mbinu (replacement)**

Ziko sababu mbali mbali ambazo zinaweza kupelekea kufanyika kwa ubadilishaji wa miundo mbinu. Kwa mfano, hali isiyoridhisha ya miundo mbinu. Mara nyingi hali hii husababishwa w na miundo mbinu iliyodumu kwa muda mrefu, teknolojia iliyopitwa na wakati, matumizi mabaya yasiyozingatia kanuni au kutokufanyia ukaguzi na matengenezo ya mara kwa mara miundo mbinu ya Chombo husika. Miundo mbinu isiyotimamu katika utendaji kazi wake yaweza kuwa na madhara makubwa ikiwa ni pamoja na kukisababishia Chombo hasara. Mathalani, upotevu wa maji pale bomba kubwa litokalo kwenye chanzo linapopasuka.

Hasara nyingine ni pamoja na upotevu wa vipuri, hujuma, kukosekana kwa utunzaji.

Uchambuzi wa miundombinu utafanyika kwa mujibu wa Kiambatisho 1 ambapo gharama ya matengezo na kukarabati kwa kila mwaka itaainishwa.

7.0 Uchambuzi wa Uwezo wa Chombo Kutoa Huduma

Uchambuzi wa uwezo wa Chombo kutoa huduma utafanyika kwa kupitia mpangilio wa kufanya kazi (Organisational Structure), idadi ya wafanyakazi na utaalamu unaohitajika.

7.3 Mpangilio wa Kufanya Kazi

Ni muhimu kupitia mpangilio wa kufanya kazi wa Chombo ili kubaini marekebisho ambayo yanapashwa kufanyika kwenye muundo. Maboresho yatapelekea kuwepo kwa ufanisi katika

kutekeleza malengo yaliyomo kwenye mpango wa kibiashara. Sehemu hii pia hubeba matokeo ya kupimia muundo wa Chombo.

7.4 Idadi ya Wafanyakazi

Chombo kitathmini idadi ya wafanyakazi wanaohitajika ili kutekeleza majukumu yake yaliyo kwenye Mpango. Marekebisho yoyote yatakayofanyika yatolewe sababu. Mapendekezo ya wafanyakazi yatafanyika kwa mujibu wa jedwali Na: 7 Nyongeza yoyote ya wafanyakazi ioane na nyongeza ya wateja waliounga maji ili kuhakikisha uwepo wa uwiano wa wafanyakazi na wateja. Izingatiwe kwamba uwiano utakuwa ni wanafanyakazi XXX kwa kila wateja XXX.



Jedwali Na. 7: Uchambuzi wa Wafanyakazi

Aina ya Watumishi	Wafanyakazi waliopo (Idadi)	Wafanyakazi Wanaohitajika (Idadi)			Maelezo ya Mabadili ko ya Idadi ya Wafanyakazi
		2021/22	2022/23	2023/24	
Uongozi (Management)					
Wasimamizi (Supervisors)					
Wafanyakazi wengine (Support staff)					
Kundi jingine la wafanyakazi (Kama wapo)					
Jumla ya Wafanyakazi					
Jumla ya Maungio ya Maji					
Wafanyakazi kwa kila maungio 1000 ya Maji Connections					

7.5 Mahitaji ya Mafunzo

Chombo kinapashwa kuchambua na kuanisha mafunzo yanayohitajika kwa kamati. atumishi watapata fursa ya kujengewa uwezo ili waweze kutekeleza mpango wa

kibiashara. Uchambuzi huo utafanyika kwa mujibu wa **Jedwali Na: 8**

Jedwali Na. 8: Uchambuzi wa Mahitaji ya Mafunzo

	Maelezo ya Aina ya Mafunzo	Gharama (TZS-Milioni)		
		2021/22	2022/23	2023/24
Kamati ya Maji				
Uongozi (Management)				
Wasimamizi (Supervisors)				
Wafanyakazi Wengine (Support staff)				
Jumla ya Gharama				



8.0 Mambo ya Kimkakati Yatakayozingatiwa Katika Mpango wa Biashara

Mambo ya msingi yatakayozingatiwa katika Mpango wa Biashara wa miaka mitatu yatawekwa bayana ili ya fahamike kwa lengo la kusaidia kuweka mipango na kufanya maamuzi. Mambo ya kuzingatiwa yataainishwa kutokana na uchambuzi uliofanyika katika vifungu Na. 4, 5, 6 na 7. Inapendekezwa, mambo ya kimkakati yawe kati ya matano na nane. Pia, kila jambo litolewe sababu kwa nini limechaguliwa kuwemo kwenye masuala ya vipaumbele. Mambo ya kimkakati yatawasilishwa kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali Na: 9



Jedwali Na. 9: Mambo ya Kimkakati

Na	Suala la Kimkakati	Sababu ya kuwa suala la kimkakati (rejea vifungu 4 hadi 7)
1	Upotevu mkubwa wa Maji	
2	Maji yanayozalishwa kutokutosheleza	
3	Uwezo mdogo wa kitaasisi (inadequate institutional capacity) hususani katika maeneo ya kamati, wafanyakazi, vifaa vya kufanyia kazi, usafiri, kompyuta n.k	
4	Kiwango kidogo cha utoaji wa huduma ya maji (Low water service coverage)	
5	Kiwango kidogo cha ukusanyaji wa mapato/ukusanyaji wa mapato usioridhisha.	
6	Ubora wa maji usioridhisha	



9.0 Malengo na Hatua za Kutatua Masuala ya Msingi ya Kimkakati

Chombo kianishe malengo yatakayofikiwa katika kutatua kila suala la kimkakati. Hatua mbali mbali zitachukuliwa kama zinavyofafanuliwa kwenye jedwali namba 10

Jedwali Na. 10: Malengo na Hatua za Kutatua Masuala ya Msingi ya Kimkakati

Na	Jambo la Msingi la Kimkakati	Lengo Mahususi	Hatua itakayofuata ili kufikia lengo	Hatua za utekelezaji zitakazochukuliwa
1	Upotevu mkubwa wa Maji	Kupunguza upotevu wa maji kutoka wastani wa asilimia 45 hadi asilimia 30 kufikia Juni 2024	Kuligawa eneo la huduma katika sehemu (Zones) mbili	Ununuzi na ufungaji wa valvu mbili zenye kipenyo cha mm 110 na uwezo wa PN 10. Ununuzi na ufungaji wa mita kubwa za maji mbili zenye kipenyo cha mm 110 na uwezo wa PN 10
			Kubadilisha mita chakavu 30 kufikia Juni 2023	Kununua na kubadilisha mita chakavu 30 zenye kipenyo cha mm 15
			Ukarabati wa mtandao wa mabomba umbali wa km 10 kufikia Juni 2023	Ununuzi wa mabomba na ulazaji wa mabomba km yenye kipenyo cha mm umbali wa km, mm.... km na mmumbali wa km
2			Kuajiri watumishi watatu kufikia June 2023	Kuajili fundi bomba wawili na Afisa ugavi mmoja.

	Uwezo mdogo wa Kitaasisi	Kuwezesha Chombo kuwa na ofisi, mitambo, usafiri na wafanyakazi wanaotoshele za kutoa huduma endelevu ifikapo 2024	Ununuzi wa pikipiki mbili kufikia Juni 2024	Ununuzi wa pikipiki mbili zenye uwezo wa 125cc
			Ujenzi wa ofisi ya CBWSO	Ununuzi wa kiwanja cha kujenga ofisi ya CBWSO huidhinishaji wa ramani na kupata vibali vya ujenzi ujenzi wa ofisi
			Ununuzi wa vitendea kazi	Ununuzi wa spanner seti moja ya Pipe Wrench.
				Ununuzi wa stock na die seti moja inayochonga bomba kuanzia mm 15 hadi 63mm
				Ununuzi wa vice ya bomba yenye uwezo wa kubana bomba kuanzia kipenyo cha mm15 hadi mm 75
3	Kiwango kidogo cha utoaji wa huduma (Low water Service Coverage)	Kuongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia hadi - 2024	Kuchimba visima vyenye uwezo wa kuzalisha jumla ya meta za ujazo 100 kwa saa	Kufanya utafiti wa kupata maeneo ya kuchimba visima Kuchimba visima, kununua pampu na kuzifunga
			Kuongeza mtandao wa bomba umbali wa km..... kufikia juni 2024	Ununuzi na ulazaji wa mabomba yenye kipenyo cha mm umbali wa kmkipenyo chamm kmmm km.....,mm kmmm km,mm -.....km

4	Kiwango kisichoridhis ha cha ukusanyaji wa mapato	Kuongeza ufanisi katika makusanyo kutoka% hadi% Juni 2024	Kununua mita za lipa kabla	Kununua na kufunga mita za lipa kabla (Hili ni jina halisi la pre pay meters?)
			Kununua mfumo wa billing wa.... na kuunganisha na GePG	Kununua mfumo wa billing na kuunganisha na GePG

10.0 Mpango Kazi (Action Plan)

Mpango kazi unatayarishwa ili kubainisha kazi zitakazofanyika ili kufikia malengo kama yalivyoainishwa katika jedwali Na: 11. Mambo yafuatayo yamefafanuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa kila lengo:

- (a) Kazi zitakazofanyika kama zilivyoainishwa kwenye jedwali
- (b) Muhusika wa utekelezaji
- (c) Ratiba ya utekelezaji
- (d) Gharama husika
- (e) Maelezo ya ziada



Jedwali Na. 11: Mpango Kazi

Lengo	Hatua zitakazofuata (Target)	Hatua za utekelezaji zitakazochukuliwa (Activity)	Mhusika	Kipindi cha kuanza kazi (Mwezi/Mwaka)	Kumaliza kazi (mwezi na mwaka)	Gharama (Million(TZS))			Aina ya Gharama (uendeshaji, matengenezo, ukarabati na uwekezaji mpya)	Chanzo cha Fedha	Maoni
						Mwaka 1	Mwaka 2	Mwaka 3			
Jumla ya Gharama											

11.0 Mpango wa Uwekezaji (Investment Plan)

Mpango wa uwekezaji unatokana na Mpango Kazi na unahusu uwekezaji katika kukarabati/ kubadilisha miundombinu na uwekezaji mpya. Taarifa za ziada za kukarabati/ kubadilisha miundombinu zinapatikana ndani ya Kiambatisho Na: 1.

Mpango wa uwekezaji utawasilishwa kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na: 12 na utakuwa na vifungu vifuatavyo:


- Lengo la uwekezaji
- Muhtasari wa uwekezaji unaolengwa
- Kipindi cha usanifu na ujenzi

(d) Gharama ya kila mwaka

(e) Chanzo cha fedha.

Jedwali Na. 12: Mpango wa Uwekezaji

Lengo la uwekezaji	Muhtasari wa Kazi Zitakazofanyika	Kipindi cha usanifu	Kipindi cha ujenzi	Mwaka-1 (Millioni TZS)		Mwaka-2 (Millioni TZS)		Mwaka-3 (Millioni TZS)		Chanzo cha Fedha
				Uwekezaji Mpya	Kubadilisha Ukarabati n	Uwekezaji Mpya	Kubadilisha Ukarabati na	Mpya Uwekezaji	Kubadilisha Ukarabati na	
Mfano: Kuongeza kiasi cha maji yanayozalishwa kutoka meta za ujazo hadi meta za ujazo.....	Kubadilisha pampu	2	3		10					Chombo



	kisima kipya	Kuchimba	3	4	20							RUWASA
			2	3			30					
	kisima Na. 3	Kufunga pampu kwenye										Chombo
SUB-TOTAL					20	10	30	15	-	-		
GRAND TOTAL					30		45		-			

12.0 Makisio ya Mahitaji ya Fedha (Mapato na Matumizi)

Makisio ya mahitaji ya fedha ya Chombo yanahusisha gharama zifuatazo:

- (O) - Gharama ya Uendeshaji (Operational Costs);
- (M) - Matengenezo (repair and maintenance cost); na
- (I) - Gharama ya Uwekezaji (rehabilitation, replacement and new investment)

$$\text{Mahitaji ya Fedha} = \text{O\&M} + \text{I}$$

12.1 Makisio ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo (O&M Costs)

Makisio ya gharama ya uendeshaji na matengenezo kwa miaka mitatu yatatokana na uchambuzi na kwa kulinganisha na gharama zilizotumika katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Makisio ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo yatawasilishwa kama ilivyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na: 13**. Aidha, Chombo kinaweza kuongeza makundi au aina ya matumizi kwa jinsi kinavyoendesha shughuli zake.


Jedwali Na. 13: Makisio ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo



Aina ya Matumizi	Gharama (TZS)						
	M-3	M-2	M-1	Mwaka wa sasa (M)	M+1	M+2	M+3
Uzalishaji Maji							
Umeme							
Madawa							
Mafuta na ilainisho							
Kutumia Maji							
Maabara							
Utunzaji wa Chanzo/vyanzo vya maji							
Kununua maji kwa ujumla							
Jumla ya Gharama za Uzalishaji							
Gharama za Usambazaji							
Umeme wa pampu (Booster Pumps)							
Mafuta na vilainisho vya generator							



Mafuta na vilainisho vya generator							
Ku test mita za wateja							
Jumla ya gharama za usambazaji							
Gharama za Matengenezo (Kutoka kwenye Jedwali...)							
Gharama za watumishi							
Mshahara							
Malipo ya vibarua							
Mcango wa mifuo ya pensheni							
Posho za kujikimu							
Jumla ya gharama za wafanyakazi							
Gharama za Utawala							
Insurance							
Umeme wa Ofisi							
Posho ya Bodi							
Gharama ya Kukagua Hesabu							
Mafunzo ya Watumishi							
Jumla ya Gharama za Utawala							



Kuimarisha utoaji huduma (Business Promotion)							
Uhusiano na mawasiliano na wateja (simu, internet n.k)							
Utoaji elimu kwa wateja							
kuweka tarifa kwenye magazeti n.k							
Jumla ya gharama za kuimarisha utoaji huduma							
Gharama zakifedha							
Gharama za benki							
Riba za benki							
Jumla ya Gharama za Fedha							
Jumla ya Uendeshaji na Matengenezo (TZS)							

12.2 Makisio ya Gharama za Uwekezaji

Makisio ya gharama za uwekezaji ni kama yalivyowasilishwa katika **Jedwali Na. 12.**

13.0 Makisio ya Bei ya Maji

13.1 Gharama za Kukidhi Uendeshaji na Uendelezaji wa Huduma za Chombo (full cost recovery)

Ili Chombo kiweze kukidhi mahitaji yake yote ya kuendesha shughuli za maji uwiano wa mapato na matumizi unapashwa kuwa kama ifuatavyo:

Mapato yatokanayo na Bei ya maji (**J**) + Mapato Mengine (**X**) = Gharama za Uendeshaji na Matengenezo (Operation and Maintenance Cost) + Uchakavu wa Miundombinu (Depreciation) + Gharama za Mtaji (Return on Investment).

Mahitaji ya Fedha ($J + X$) = O&M + D + I


Mapato mengine yanaweza kutokana na:

- Kurudisha maji yaliyokatwa
- Kuunga maji
- Msaada kutoka serikalini/Ruzuku

Gharama ya uchakavu wa miundombinu ni kwa ajili ya kukarabati miundombinu na gharama ya mtaji ni kwa ajili ya uwekezaji mpya. Ili kuweza kukokotoa gharama ya uchakavu na mtaji inabidi thamani ya miundombinu (asset value) pamoja na utaratibu wa kuainisha uchakavu wa “Assets” (depreciation Schedule) ufahamike. Suala hili linasisitizwa kwa waratibu wa vyombo japo kwa hali ilivyo hivi sasa sio rahisi kwa vyombo kuainisha baadhi ya taarifa kwa usahihi.

Kanuni Mbadala ya Mahitaji ya Fedha

Kutokana na changamoto ya kupata taarifa sahihi na za



kuaminika za thamani ya mali (asset value) kwenye vyombo vya maji vya kijamii, Chombo kitakokotoa mahitaji ya fedha ya kukidhi gharama zote za uendeshaji na uendelezaji wa huduma za maji sawa na asilimia 150 (150%) ya gharama ya uendeshaji na matengenezo. Kanuni itasomeka kama ifuatavyo:

$$\text{Jumla ya Mahitaji ya Fedha} = 150\% \times \text{Matengenezo na Ukarabati (O\&M Costs)}$$

Kanuni hii ya ukokotoaji wa bei za maji inatumiwa na **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji ya Kenya (WASREB)** na **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji Zambia (NWASCO)**. Kanuni hii imefikwa baada ya utafiti wa muda mrefu walioufanya na ambao uliithibitisha kanuni hiyo. Kwa mantiki hiyo, Chombo kitakidhi 100% ya gharama za uendeshaji na matengenezo na 50% yake itakidhi gharama ya uchakavu (kwa ajili ya kukarabati miundombinu) na mtaji (kwa ajili ya uwekezaji).

Kwa kuzingatia matakwa ya kanuni hii, Chombo kitatengeneza ratiba (roadmap) ya kuhakikisha mapato yake yanakua kuelekea kukidhi asilimia 150 ya gharama ya uendeshaji na matengenezo.

Gharama ya uendeshaji na matengenezo inapatikana kwa mujibu wa **jedwali Na. 13**, na gharama ya ukarabati na uwekezaji itapatikana kwa mujibu wa **jedwali Na. 12**.

13.2 Makisio ya Mapato na Uchambuzi wa Bei ya Maji

Mapato yanayopashwa kutokana na bei (mauzo) ya maji (J): (Gharama zote za uendeshaji chombo (A)) – (Mapato mengine. (X)). Makisio ya mapato yatakatokana na bei (mauzo) ya maji na uchambuzi wa bei vimeonyeshwa kwenye jedwali Na: 14 hapa chini.

Jedwali Na. 14: Makisio ya Mapato na Uchambuzi wa Bei

Maelezo	Mwaka wa Sasa (M)	M+1	M+2	M+3
Gharama za kukidhi uendeshaji wa Chombo (A) TZS				
Mapato mengine (X) TZS				
Mapato yatakayotokana na bei ya maji (J)=(A-X) TZS				
Maji yanayotegemewa kuzalishwa/mwaka (P) m3 rejea Jedwali				
Maji yatakayopotea (N)%				
Maji yanayotegemewa kufikia wateja (L)=P-N m3				
Wastani wa Bei ya maji (Q) =J/L TZS /m3				



13.3 Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Watumiaji wa Maji

Ili kuainisha bei tofauti kwa makundi mbali mbali (differential tarifa) ya watumiaji maji inabidi kutafuta uwiano wa matumizi ya maji kati ya makundi ili kuweza kutofautisha bei ya maji kati ya makundi hayo. **Jedwali Na: 15** inaonyesha mfano wa uwiano wa matumizi ya maji kwa makundi ya viosk, Nyumbani, Taasisi na Biashara.



Jedwali Na. 15: Uwiano wa Matumizi ya Maji kwa Makundi

Aina ya Matumizi	Uwiano wa Matumizi ya Maji kwa Makundi			
	Mwaka wa Sasa	Mwaka 1	Mwaka 2	Mwaka 3
Matumizi ya Vioski	10%	12%		
Matumizi ya Nyumbani	75%	73%		
Matumizi ya Taasisi	15%	13%		
Matumizi ya Biashara	5%	2%		
Jumla	100%	100%		

Kwa kutumia uwiano wa matumizi ya maji unaweza kuweka bei tofauti kwa makundi mbali mbali. Kwa mfano viosk na matumizi ya nyumbani wanaweza kulipa chini ya wastani ambapo watafidiwa na makundi mengine kama biashara, taasisi ambayo yatalipa zaidi ya wastani maadam mapato yatakayotokana na mauzo ya maji yabaki vile vile.

Kwa wateja wasio na dira ya maji watalipa kwa kulingana na makadirio ya matumizi yao ukizidisha na bei ya kundi lake.

13.4 Kuoanisha Bei ya Maji na Uwezo wa Kulipa


Ikionekana bei ni kubwa au ongezeko la bei ni kubwa ikilinganishwa na uwezo wa wateja kulipa, punguza mapato yanayotegemewa kutoka kwenye bei ya maji mpaka ufikie bei muafaka. Kiasi kitakachopunguzwa kiwe kwenye gharama ya uchakavu na ukarabati'. Vyombo vinapashwa vihakikishe kuwa bei itayopendekezwa inakidhi gharama ya uendeshaji na matengenezo kwa aslimia 100%.

13.5 Mapendekezo ya Bei ya Maji

Mapendekezo ya bei ya maji kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Biashara yataainishwa kwa mujibu wa jedwali Na: 16 Pia Jedwali hili linatoa fursa ya kulinganisha bei pendekezwa, bei iliyopo na zile za nyuma yake. Hii husaidia pia kutathmini kama bei pendekezwa imeongezeka sana (Rejea 13.4).

Jedwali Na. 16: Mapendekezo ya Bei ya Maji

Bei ya Maji	M-3	M-2	M-1	Mwaka wa sasa (M)	M+1	M+2	M+3
Viosk							
Majumbani							
Taasisi							
Biashara							
Viwanda							
Kurudisha maji							
Viosk							
Majumbani							
Taasisi							
Biashara							
Viwanda							
Kuunga Maji							
Jumala ya gharama za Usambazaji							
Bei Nyinginezo							



14.0 Kupitisha Mpango wa Biashara

Mpango wa Biashara wa Chombo ni lazima upitishwe na Kamati ya Maji katika kikao halali na usainiwe na Mwenyekiti na Katibu.

15.0 Utekelezaji wa Mpango wa Biashara

Ili kuhakikisha kuwa Mpango wa Biashara unatekelezwa ipasavyo, kila bajeti ya Chombo kwa miaka ambayo iko ndani ya mpango husika inapashwa kutokana na muongozo huo. Endapo kutakuwepo na mabadiliko makubwa itabidi kwanza kuupitia na kuurekebisha mpango kabla ka kutengeneza bajeti.

Pia, mpango huu ndio utakuwa msingi wa RUWASA kupitia na kupitisha bei za maji zitakazokuwa zinaombwa na Chombo.


Mpango wa Biashara ni nyaraka muhimu, kwa hiyo Chombo kiweke utaratibu kutathmini utekelezaji wake kila baada ya robo mwaka. Utaratibu wa kutathmini utabainishwa kwenye Mpango.



16.0 Viambatisho

16.1 Kiambatisho Na 1: Tathmini ya Miundombinu na Gharama za Kurekebisha


a N	Aina ya Miundombinu na Maelezo yake	Mahali Ilipo	Idadi	Hali ya Miundo mbinu kwa Sasa Inaridhi sha/ Hairidhi shi	Hali ya Miundombinu na Gharama za Kuirekebisha					
				Inaridhisha			Hairidhishi			
				Gharama za Matengenezo (TZS)			Gharama za Kukarabati/ Kubadilisha (TZS)			
				M	M+1	M+2	M+3	M+1	M+2	M+3
	1	2	3		4	6	7	9	10	11
1	Miundo Mbinu ya Uzalishaji Maji									
2	Miundo mbinu ya vyanzo									
3	Visima (Boreholes) . (Urefu na Kipenyo)									
4	Mabwawa (Ujazo)									
5	Mitambo ya kusafisha na kutibu maji(Aina na uwezo)									
6	Vifaa vya maabara									



7	Matanki ya maji (clear water tanks) . (Aina (ya zege/chuma) ,ujazo, na kama ni' Raiser' kwa mita ngapi au									
8	Bomba za Njia Kuu ya Maji (Transmission Mains) (Aina na Kipenyo)									
9	Pampu na Vifaa vyake(Aina na uwezo wake-elezea kama ni "sub-mersible au surfacepump ')									
10	Mita za kupima kiasi cha maji yanayozalishwa(Aina na Kipenyo)									
11	Miundo Mbinu ya Usambazaji Maji									
12	Bomba za kusambaza maji ('Distribution Mains') (Aina na Kipenyo)									



13	Matanki ya maji (Aina (la zege/chuma) , Ujazo, na kama ni' Raiser' kwa Surface Tank 'mita ngapi									
14	Pampu za kuongeza msukumo wa maji "Booster Pumps and other peripherals" (Aina na uwezo wake)									
15	Valvu(Kipeny o)									
16	Dira za maji za wateja (Customer Meters) (Kipenyo)									
17	Valvu za kutolea maji ya kuzima oto (Fire Hydrants)									
18	MISCELLANEOUS									
19	Ardhi ya Chombo (Maelezo ya ukubwa, Plot na block numbers kama imepimwa									



20	Majengo (maelezo ya jengo na ukubwa wake)									
21	Samani kama vile meza viti n.k									
22	Baisikeli									
23	Piki piki, aina na cc zake									
24	Magari, aina na cc zake									
25	Computers and accessories elezea kama ni "Laptops au Desktops"									
26	Vifaa vya ofisi air conditioners Refrigerators									





Guidelines on Regulation of Community Water Service Management



NBC Bank, Mazengo Branch, Kuu Road,
P. O. Box 412, 40473 Dodoma,
Tanzania
Phone: +255 2323563/4
Email: dg@ruwasa.go.tz